TANGAZO LA SERIKALI NA. 688 la tarehe 15/9/2023

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
SURA YA 290

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA (ADA NA VIBALI VYA BURUDANI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA YA MWAKA 2023

Jina

TS Na.560
16/9/2022

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ada na Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2023, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ada na Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya Kifungu cha 4

2. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 4(2) cha Sheria Ndogo Kuu kwa kukifuta na kukiandika upya ili kisomeke kama ifuatavyo:

   "2 Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika Kifungu Kidogo cha (1) kibali hicho kitaombwa kwa kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii ".

Marekebisho ya Kifungu cha 8

3. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 8 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kuongeza Jedwali la Tatu ili lisomeke kama ilivyooneshwa katika Sheria Ndogo hii.

Marekebisho ya Kifungu cha 10

4. Marekebisho yamefanyika katika Kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo Kuu kwa kubadilisha rejea ya Jedwali la Tatu na badala yake lisomeke kuwa rejea ya Jedwali la Nne.

Marekebisho ya Jedwali la Pili

5. Marekebisho yamefanyika katika Jedwali la Pili katika kipengele cha 11 kwa kuweka muda ili usomeke "kwa kila tukio ".

JEDWALI LA TATU

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 8)

KIBALI CHA KUFUNGA BARABARA

SEHEMU YA KWANZA

(Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la mwombaji<br><br>............................................................ | 2. Anwani ya mwombaji<br><br>......................................... |
| 3. Aina ya sherehe<br><br>............................................................. | 4. Eneo analokusudia kufanya sherehe<br><br>............................................ |
| 5. Muda wa kuanza<br><br>............................................................ | 6. Muda wa kumaliza<br><br>.................................................... |
| 7. Ada ya kibali (Shilingi)<br><br>......................................................... | 8. Namba ya Stakabadhi ya malipo<br><br>................................................ |
| 9. Saini……………………………… | 10. Tarehe………………….... |

SEHEMU YA PILI

(Kwa Matumizi ya Ofisi tu)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi namba<br><br>..................................... | 2. Ada ya kibali Shilingi<br><br>....................................................... |
| 3. Namba ya stakabadhi ya malipo<br><br>.................................................. | 4. Tarehe ya malipo<br><br>....................................... |
| 5. Jina la Afisa aliyepokea malipo<br><br>................................................... | 6. Saini<br><br>...................................... |
| 7. Muhuri | |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*futa isiyohusika*)

Sababu: ………………………………..…………………………………………

Jina:………………………………Saini: ……………Tarehe………………..

Dodoma,
Agosti, 2023

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI (MB)
*Waziri wa Nchi - Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*